JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

TANGAZO LA FURSA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KWA KOZI ZA MUDA MREFU KATIKA VYUO VYA VETA KWA VIJANA WANAOTOKA KATIKA MAZINGIRA MAGUMU KUPITIA MPANGO WA UFADHILI WA MFUKO WA KUENDELEZA UJUZI (SKILLS DEVELOPMENT FUND – SDF) KWA MWAKA 2027.

1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (Skills Development Fund – SDF), inawatangazia vijana wanaotoka katika **Mazingira magumu** kuhusu fursa za kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi ya muda mrefu katika vyuo vya VETA kwa mwaka wa masomo 2027, kupitia Mpango wa Ufadhili wa Mafunzo (Bursary Scheme).

Mpango huu unalenga kuwawezesha vijana wenye uhitaji kupata elimu, ujuzi na maarifa yatakayowaongezea uwezo na fursa za kupata ajira, kujiajiri na kujitegemea kiuchumi.

2. SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;

i. Mtanzania mwenye Umri kuanzia miaka 15 hadi 35.
ii. Ajue kusoma na kuandika.
iii. Anayetoka katika mazingira magumu.

3. UTARATIBU WA KUOMBA

i. Maombi yatawasilishwa kwa njia ya mtandao (Online Application) kupitia mfumo wa maombi unaopatikana kwenye tovuti ya VETA (www.veta.go.tz) au kwa kujaza fomu za maombi za nakala ngumu (Hardcopy), zitakazopatikana katika chuo cha VETA kilicho karibu nao.

ii. Fomu zote za kujiunga zinatolewa bure kwa kuwa zimegharamiwa na Serikali.

iii. Mwombaji anatakiwa kuwasilisha fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu, ikiambatishwa na nyaraka zifuatazo:

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- Nakala za vyeti vya elimu aliyonayo;
- Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa au Afisa Maendeleo ya Jamii, namba ya utambulisho wa TASAF au barua ya utambulisho kutoka SHIVYAWATA au barua ya utambulisho kutoka NACOPHA kwa ajili ya kuthibitisha kuwa mwombaji anatoka katika mazingira magumu; na
- Picha ndogo tatu (3) za mwombaji zenye mandhari nyuma ya rangi ya bluu.

4. KIPINDI CHA MAOMBI

Fomu zitatolewa kuanzia tarehe **10 Novemba, 2026** na mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni tarehe **20 Novemba, 2026.**

5. ADA NA GHARAMA ZA MAFUNZO

Gharama za ada ya mafunzo zitagharamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF).

NB: Orodha ya vyuo vya VETA pamoja na fani zitakazotolewa kwa mwaka wa masomo 2027 imeambatishwa katika tangazo hili.

Kwa Maelezo na Ufafanuzi zaidi, wasiliana nasi:
VETA Makao Makuu,
12 Barabara ya VETA, 41104 Tambukareli, S. L. P. 802, Dodoma
Barua pepe: info@veta.go.tz au pr@veta.go.tz
Simu: +255 26 2963661
Simu ya mkononi: 0755 26 74 89

UFUNDI STADI, FURSA KAMA ZOTE KWA WATU WOTE